EXAMINATION NUMBER.....

MBEZIBWA THE GREAT ACADEMIC PLATFORM

MTGAP BRELA-REGI. NO. **613055.**

Mbezibwaemmanuel2@gmail.com

mbezip@gmail.com

CONTACTS

0758764778, 0758723120, 0750208434, 0678474807

MIPANGO STREET,DODOMA –TANZANIA

MTIHANI MAALUM KANDA YA KUSINI.

(LINDI, MTWARA AND RUVUMA)

KISWAHILI-01

Muda: Saa 1: 40 Jumatatu 20 APRILI 2026.

MAELEKEZO:

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, na C zenye jumla ya mswali sita (6)
2. Jibu maswali yote kwenye nafasi ulizopewa
3. Sehemu A na B zina alama ishirini (20) kila moja na sehemu C ina alama kumi (10)
4. Majibu yote yaandikwa kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi, isipokuwa katika michora ambapo ni lazima kutumia penseli
5. Andika namba yako ya mtihani na taarifa zote muhimu hapo juu

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU		
NAMBA YA SWALI	ALAMA	SAHIHI YA MTAHINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
JUMLA		
SAHIHI YA MHAKIKI		

EXAMINATION NUMBER.....

SEHEMU A (20 MARKS)

1. **Sikiliza kwa makini hadithi utakayosomewa na msimamizi, kisha jibu kipengele cha (i) – (v), kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku.**

(i) Hadithi uliyosikikiliza inahusu nini?

A. Kinyonga C. Wanyama E. Binti mrembo
B. Riadha D. Sherehe

(ii) Kinyonga aliibuka kidedea katika mchezo gani?

A. Kucheza C. Riadha E. Mpira wa miguu
B. Kuruka D. Kuogelea

(iii)Nahau „kuasi ukapera" kama ilivyotumika katika hadithi hii ina maana gani?

A. Kuoa C. Kukimbia E. Kujipatia umaarufu
B. Kulewa pombe D. Kuwa mwangalifu

(iv) Nini kilimtokea kinyonga baada ya kulewa pombe na kisha kucheza kwa kasi ya ajabu pale ukumbini?

A. Aliwaangukia wakwe zake D. Alianza kucheza taratibu
B. Alizomewa na wakwe zake E. Aliondoka ukumbini na kuelekea nyumbani
C. Alimkosa binti mrembo

(v) Ni funzo gani linapatikana katika hadithi uliyosikiliza?

A. Ni vizuri kuepuka umaarufu
B. Si vizuri kuwa na mafanikio katika maisha
C. Kulewa pombe huleta uchangamfu
D. Ni vizuri kucheza kwa kasi unapokuwa kwenye sherehe E. Unapofanya jambo fulani kuwa makini

2. **Kuanzia swali la (i)-(x), chagua jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku.**

(i) Bahati aliuliza kuwa kwanini magari hayapiti pale siku hizi? Hii ni kauli gani ya usemaji?

A. Halisi C. Taarifa E. Tata
B. Changamano D. Sahili

(ii) Ndege mweupe ametua <u>juu ya mti</u> mkubwa. Maneno yaliyopigiwa mstari ni aina gani ya maneno?

A. Nomino ya kawaida C. Kitenzi kishirikishi E. Kiunganishi
B. Kihusishi D. Kielezi cha mahali

(iii)Wanafunzi wa darasa la saba wanakaribia kufanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi. Sentensi hii ipo katika nafsi gani?

A. Nafsi ya kwanza wingi D. Nafsi ya pili wingi
B. Nafsi ya tatu wingi E. Nafsi ya pili umoja

C. Nafsi ya tatu umoja

(iv) Baba Ivan hajavuna mpunga mwingi msimu huu kwa sababu hakutumia pembejeo bora za kilimo. Sentensi hii ipo katika hali gani?

A. Mazoea C. Endelevu E. Timilifu
B. Ukanushi D. Isiyodhihirika

(v) Baba mwenye nyumba ameamua kumtia ndani mpangaji wake kutokana na ukorofi wake. Nini maana ya nahau „tia ndani‟ kama ilivyotumika katika maelezo haya?

A. Fungia ndani C. Weka mahabusu E. Funga mikono
B. Angika juu D. Ingiza chumba cha ndani

(vi) Ukumbi wetu **umepambika** vizuri. Neno „umepambika‟ likiwa katika kauli ya kutendwa huwa neno gani kati ya haya yafuatayo?

A. Umepandwa C. Umepambiwa E. Umepambia
B. Umepambishwa D. Umepambwa

(vii) Kamilisha kitendawili hiki: Nimelala ila nachungulia_____

A. Nje C. Sinema E. Juu
B. Kabuli D. Ndoto

(viii) Pamela ana tabia ya kumwaga chakula kinachobaki baada ya kushiba. Je utatumia methali ipi kati ya zifuatazo kumshauri Pamela aache tabia hiyo?

A. Nyongeza haigombi D. Mwenye shibe hamjui mwenye njaa
B. Akiba haiozi E. Haba na haba hujaza kibaba
C. Usiache mbachao kwa msala upitao

(ix) Bibi anapenda kutumia sufuria kupikia mboga za majani. Upi ni wingi wa neno sufuria kati ya maneno haya?

A. Sufuria C. Masufuria E. Lisufuria
B. Visufuria D. Misurufia

(x) Kijiji cha Songambele kimekumbwa na _____la njaa kutokana na ukosefu wa mvua kwa muda mrefu. Neno lipi linakamilisha sentensi hii?

A. Jangwa C. Jaa E. Lindi
B. Baa D. Ukame

3. **Oanisha maelezo yaliyopo katika Orodha A na maneno yaliyopo katika Orodha B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika mabano**

Na.	Orodha A	Majibu	Orodha B
(i)	Usiposoma kwa bidii mambo yatakuwa…….na kufanya usiwe na mafanikio.	( )	A. Bakaya.
(ii)	Kumi na Mbili.	( )	B. Mgwisho.
(iii)	Mbezi alionesha ……..wake kwa kupambana na chui.	( )	C. Lisanji
(iv)	Kikembe cha Fisi	( )	D. Ugeesi.
(v)	Babu yake alitumia …….uliokuwa wa ng'ombe kupunguza inzi kwenye kidonda.	( )	E. Thenashara
			F. Kifisi
			G. Benibeni.

SEHEMU B (ALAMA 20)

4. Soma na upange sentensi zifuatazo katika mtiririko sahihi kwa kutumia herufi A, B, C, D na E

i. Kumbe alikuwa ni mama yangu mzazi [ ]
ii. Nikakaa kwenye sofa na kuwasha runinga [ ]
iii. Aliponiona akanikumbatia kwa furaha huku akinipa pole ya safari [ ]
iv. Ghafla nikasikia mchakacho kutokea jikoni ukija sebuleni [ ]
v. Kisha nikamsimulia yote yaliyojiri kwenye safari hiyo yakutisha [ ]

5. Soma habari hii kisha jibu kipengele cha i hadi v.

Umaskini hauwezi kuondolewa kwa maneno matupu kama vile kukemea au kutangaza katika vyombo vya habari. Tunaweza kuondoa umaskini kwa kufanya kazi kwa bidii na maarifa.

Ni kazi bure kwa mkulima kuendelea kufyeka mashamba mapya kila mara kwa matarajio ya kuvuna mazao mengi bila mpangilio. Kwani kilimo kinahitaji mkulima awe na juhudi ya kulima na awe na maarifa ya kutumia ardhi kwa faida. Hata hivyo kilimo cha jembe la mkono hakitamuondolea mkulima umaskini ila kitaendelea kumchosha, kumzeesha na kumfanya maskini maisha yake yote. Mkulima ni lazima abadili fikra zake kuhusu kilimo cha kutumia jembe la mkono, hivyo afikirie njia ya kulima kwa kutumia jembe la kukokotwa na wanyama ambao tunao, kwa kufanya hivyo tunaweza kulima shamba kubwa tena kwa muda mfupi.

Mkulima wa kisasa ashauriwe kupanda mbegu bora kwani akipanda mbegu zisizo bora asitarajie kuvuna mazao bora na mengi hata kama mvua zitanyesha vizuri. Mbegu bora hutoa mazao bora. Mkulima anashauriwa apande kwa nafasi, apalilie kwa wakati, aue wadudu waharibifu wa mazao shambani kwa kufuata ushauri wa mtaalamu wa kilimo. Atumie mbolea ya samadi kwani ni nzuri kwa kilimo. Hapo atapata mavuno bora na kuushinda umaskini.

MASWALI

i. Kilimo cha jembe la mkono kinaweza kuleta athari hasi nyingi kwa mkulima. Je, kwa mujibu wa habari hii ni athari hasi ngapi zinazotajwa zinazoweza kuletwa na kilimo cha jembe la mkono?_____
_____

ii. Ili tuweze kuondoa umaskini, tunashauriwa mambo muhimu ya kuzingatia katika suala la kilimo. Kwa mujibu wa habari, wewe kama mtaalamu wa maendeleo unashauri wananchi wafanye nini kuhusu kilimo chao? (jibu lako lisizidi maneno manne)_____

iii. Umepewa sentensi tano ambazo zinazungumza habari ya kilimo bora zaidi. Chagua sentensi moja na uiandike inayokamilisha utaratibu bora zaidi wa kilimo cha kisasa Kupanda kwa nafasi na kupalilia kwa wakati. Matumizi ya pembejeo za kilimo. Kuzingatia maandalizi ya shamba. Kanuni bora za kilimo.Kanuni bora za mazao

iv. Wafuatao waweza kuwa waandishi wa habari hii. Lakini unafikiri ni nani zaidi angefaa kuwa mwandishi wa habari hii Mtanzania, Mwalimu, Mkulima, Mwananchi, au Mzalendo?_____

v. Maneno yafuatayo yanaweza kuwa vichwa vya habari kwa habari uliyoisoma. Je, ni neno gani lina uzito zaidi kuhusiana na habari uliyoisoma? MKULIMA, UMASKINI, KILIMO, PEMBEJEO._____

SEHEMU C (ALAMA 10).

6. Soma kwa makini tangazo la biashara lifuatalo kisha jibu maswali yafuatayo chini.

HUDUMA YA MITIHANI KWA BEI YA KUSHANGAZA.

Unahitaji huduma ya mitihani yenye ubora wa hali ya juu kwa bei ya kushangaza?

Tembelea ofisi za Mbezibwa The Great Academic Platform leo

- **Tunatoa mitihani mipya yenye thamani halisi inayoendana na mtaala mpya na fomati mpya .**
- **Nukuu za masomo yote**
- **Maazimio ya kazi**
- **Vitabu vya kujifunzia vya ziada.**
- **Mitihani mbalimbali tunaandaa**
- **Tuaandika maandiko ya kibiashara.**

Mahali; Jijini Dodoma karibu na Chuo cha Mipango

Mawasiliano; 0758 -723-120, 0758-764-778.

Website. www.mbezibwathegreat.co.tz

Barua pepe; mbezibwaemmanuel2@gmail.com

Mbezibwa The Great Academic Platform

"Platfomu bora kwa kazi Bora".

Maswali

A. Tangazo linahusu bidhaa gani kuu?_____
B. Tangazo linatambulisha Ofisi ziko wapi?_____
C. Ni kauli mbiu ipi imetumika katika tangazo hili?_____
D. Taja huduma zinazotolewa zilizoandikwa kwenye tangazo_____
_____
E. Yapo mambo kadhaa ya kuzingatia wakati wa uandishi wa tangazo la biashara.Taja mambo mawili
(i)_____
(ii)_____

EXAMINATION NUMBER.....

MBEZIBWA THE GREAT ACADEMIC PLATFORM

MTGAP

DODOMA-TANZANIA

0758-723-120 / 0758 764-778

HABARI YA KUSIKILIZA MTGAP KISWAHILI-APRILI 2026

Karne nyingi zilizopita kinyonga alikuwa mnyama mwenye mwendo kuliko wanyama wengine. Mara nyingi aliibuka kidedea katika mashindano ya riadha. Jambo hili lilimletea umaarufu mkubwa na kupendwa na wasichana wengi. Hatimaye kinyonga, alijipatia binti mmoja mrembo na kuamua kuasi ukapera.

Maisha yake yalijaa mafanikio makubwa. Siku moja alialikwa na wakwe zake kwenye sherehe iliyokuwa imeandaliwa. Bwana kinyonga na marafiki zake walilewa pombe siku hiyo. Kinyonga alianza kucheza ukumbini kwa kasi ya ajabu. Kwa bahati mbaya alishtuka amewaangukia wakwe zake. Looh! Kinyonga aliona aibu na kuanzia siku hiyo alianza kutembea kwa makini na taratibu.

EXAMINATION NUMBER.....

TO ALL TEACHERS AND EDUCATION STAKEHOLDERS

Mbezibwa The Great Academic Platform (MTGAP) is a platform registered with the Government of Tanzania under BRELA registration number 613055 and fully licensed to carry out education related activities in Tanzania ,including holding the required operational licenses.We are pleased to announce that we will soon begin administering examinations to English Medium Primary schools ONLY mainland Tanzania.This is a valuable opportunity for pupils to assess their academic performance at higher standard. FEE; 5000 per Pupil.

We are inviting a limited number of english medium Primary schools only in order to maintain our standard of excellence,in line of our motto "QUALITY OVER QUANTITY" Slots are limited register now.

The Platform is mainly focused on the preparation and development of examinations and the writing of Academic Project proposal and Business project propal, Academic books for primary and secondary schools in Tanzania.These materials are designed to serve as supplimentary and refference books for learning.

In additional MTGAP is also engaged in production of religious books storrybooks,and professional development books for workers in both formal and informal sectors in Tanzania.
We hereby invite all Education stakeholders across Tanzania.We prepare all types of Examination classes under both the Revised curriculum and the Former curriculum both Swahili and English as mode of communication.

Our services are affordable and cost-friendly, with the aim of improving Academic performance and supporting schools that collaborate with us.
We prepare the following examinations;

- Standard 4 and 7 Examination
- Weekly tests
- Mid term Examinations
- District Mock Examinations
- Regional Mock Examinations
- Terminal Examinations
- Joint Examination
- Ward Mock Examinations

Call us today to press your order.
We are located in Dodoma City near the Collage of Institute of Rural Development.For Inquiries contact The CEO Mbezibwa The Great Academic Platform Phone +255 758-723-120,+255 758-764-778,+255 750 208-434, +255 673-788-679 (WASAP NO +255 712-393-104,+255 758 764-778) Email mbezibwaemmanuel2@gmail.com

Payment information; All Payments should be made via Vodacom LIPA NUMBER 3665538I
Account Name Mbezibwa The Great.